HOTUBA YA MHESHIMIWA BENEDICT NGALAMA OLE NANGORO (MB), NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI KWENYE UFUNGUZI WA MKUTANO WA TATU WA BARAZA LA MWAKA LA WADAU WA SEKTA NDOGO YA NYAMA TANZANIA, ST. GASPAR, DODOMA, TAREHE 13/01/2011

Ndugu Mwenyekiti wa Mkutano huu
Ndugu Katibu Mkuu Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi,
Ndugu Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi
Ndugu Mwenyekiti wa Baraza la Mwaka la Wadau wa Sekta ndogo ya Nyama,
Ndugu Mwenyekiti wa Bodi ya Nyama Tanzania,
Ndugu Msajili wa Bodi ya Nyama,
Ndugu Wawakilishi wa Wizara na Taasisi za Serikali,
Ndugu Wawakilishi wa Taasisi zisizo za Kiserikali (NGO),
Ndugu wajumbe wa Baraza la Mwaka la Wadau wa Sekta ndogo ya Nyama,
Ndugu wajumbe wa Bodi ya Nyama Tanzania,
Wageni Waalikwa,
Mabibi na Mabwana.

Ndugu Mwenyekiti, awali ya yote, ninayo furaha kubwa sana kuwa pamoja nanyi siku ya leo, katika ufunguzi wa mkutano huu wa muhimu kwa maendeleo ya sekta ya mifugo hususan maswala ya nyama nchini. Napenda nichukue fursa hii kuwapongeza na kuwashukuru waandaaji wa mkutano huu kwa kunialika kuja kuifungua.

Aidha, nawashukuru wenyeji wetu wa mkoa wa Dodoma kwa kukubali kuwa wenyeji wa mkutano huu kwa mara nyingine na kwa mapokezi mazuri ya wadau waliohudhuria katika mkutano huu. Tatu napenda kuzipongeza Halmashauri za Wilaya zilizowezesha wajumbe wake kushiriki katika mkutano huu muhimu na ninashauri Halmashauri nyingine kuiga mfano huu.

Ndugu Mwenyekiti, napenda kuwapa pole washiriki wa mkutano kwa kusafiri kutoka mbali, lakini pia kuwashukuru kwa kukubali kuja kushiriki nikiamini kuwa mmefanya hivyo kwa kutambua umuhimu wa mkutano huu na nafasi yake katika kuleta mabadiliko endelevu katika sekta ndogo ya nyama nchini katika jitihada za kuleta ufugaji wenye tija.

Ndugu Mwenyekiti, baraza lina jukumu la kusimamia utekelezaji **wa Sheria ya Nyama Na. 10 ya Mwaka 2006** pamoja na sheria nyingine zinazoongoza sekta ya nyama ikiwa ni pamoja na Sheria ya Usalama wa Chakula, **Madawa na Vipondozi Na 1 ya Mwaka 2003, Sheria ya Magonjwa ya Mifugo Na. 17 ya Mwaka 2003, Sheria ya Ngozi Na 18 ya Mwaka 2008**, **Sheria ya Ustawi wa Wanyama Na. 19 ya Mwaka 2008, Sheria ya Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa Mifugo na Mazao yake Na.12 ya Mwaka 2010, Sheria ya Nyanda za Malisho na Vyakula vya Mifugo Na. 13 ya Mwaka 2010 ni muhimu ili kuhakikis**ha sekta inaendeshwa kwa utaratibu wenye tija. Pamoja na majukumu hayo, **Baraza hili linapaswa kufanya kazi kwa kuzingatia Sera ya Mifugo ya mwaka 2006 na Mkakati wa kutekeleza sera hiyo.**

Ndugu Mwenyekiti, nimeambiwa kuwa huu ni mkutano wa kisheria na ni wa tatu tangu Baraza hili lizinduliwe. Maudhui ya mkutano ni: 1) kutathimini utekelezaji wa yale yaliyoelekezwa katika mkutano wa pili wa Baraza hili uliofanyika mwezi Februari 2010; 2) kushirikishana uzoefu pamoja na kuainisha changamoto zilizojitokeza wakati wa kutekeleza majukumu yenu ili zijadiliwe na kupatiwa ufumbuzi; 3) kuyapitia upya mikakati iliyopo na kujipanga vizuri kwa kipindi ninachokuja, 4) kuhuisha mikakati ya sekta ndogo ya nyama na programu nyingine zinazoendelea hasa ile ya Kilima/Mifugo/Uvuvi Kwanza pamoja na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya 2010.

Ndugu Mwenyekiti, Tanzania ina raslimali kubwa ya mifugo na ni nchi ya tatu kwa wingi wa mifugo katika Afrika ikitanguliwa na nchi Ethiopia na Sudan. Hivi sasa Tanzania inakadiriwa kuwa na ng'ombe milioni **19.2,** mbuzi milioni **13.7,** Kondoo milioni **3.6,** nguruwe milioni **1.9** na kuku milioni **58** ambayo inachangia katika kumpunguzia mwananchi umaskini. Aidha, tunafahamu kuwa mifugo yote inalenga kuzalisha zao la nyama ukiondoa ng'ombe wa maziwa wapatao **608,000** na kuku milioni **7** wa mayai ambao pia huzalisha nyama. Takwimu za uzalishaji wa nyama na biashara ya mifugo zinaonyesha kwamba takriban ng'ombe **857,208**, mbuzi **682,992** na kondoo **112,035** waliuzwa kwenye minada hapa nchini katika mwaka 2009/2010 na kuzalisha wastani wa tani **449,673** za nyama, kati ya hizo tani **243,943** ilikuwa nyama ya ng'ombe, tani **82,884** nyama ya mbuzi na kondoo, tani **38,180** ya nguruwe na tani **80,916** nyama ya kuku. Uzalishaji huu ni mdogo ukilinganishwa na rasilimali

zilizopo nchini na unasababisha ulaji mdogo wa nyama unaokadiriwa kuwa **kilo 12** kwa mtu kwa mwaka ikilinganishwa na kilo 50 zinazopendekezwa na FAO.

Aidha, katika kipindi hicho Tanzania imeuza ng'ombe **2,970,** mbuzi na kondoo **302** kwenda nchi za Comoro, Kenya na Burundi. Biashara ya nyama nje ya nchi inashamiri ambapo nchi yetu imeuza jumla ya **tani 193.5** za nyama ikiwa ni **tani 36.9** za nyama ya ng'ombe, **tani 122** za nyama ya mbuzi na **tani 34.6** za nyama ya kondoo kwenda nchi za Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE), Kuwait, Oman, Jamhuri ya Demokrasia ya Kongo (DRC) na Malawi kiasi ambacho ni kidogo ikilinganishwa na rasilimali ya mifugo iliyopo.
Ndugu Mwenyekiti, pamoja na utajiri huu mkubwa wa raslimali ya mifugo, bado uzalishaji, uvunaji na mauzo ya mazao ya mifugo, hususan maziwa, ngozi na nyama ni duni sana nchini. Sababu za uduni huu ni pamoja na ukosefu wa ardhi, malisho na maji ya kutosha; uhaba wa miundombinu ya masoko; uhaba wa huduma za tiba na udhibiti wa magonjwa; wadau kutokuwa na habari za kutosha juu ya mahitaji ya soko la nyama k.m ladha ya nyama ipendwayo na soko, kiasi sahihi cha mafuta kwenye nyama na kukatwa kwa kiasi na jinsi walaji wanavyotaka. Aidha, ukosefu wa machinjio ya kisasa ya kutosha na viwanda vya kusindika nyama navyo vimechangia kudumaa kwa ufanisi wa sekta ndogo ya nyama nchini. Tatizo sugu la ukame pia limeripotiwa kuchangia sana katika ufanisi mdogo wa sekta ndogo ya nyama.

Pamoja na changamoto hizi, sekta ndogo ya nyama imeendelea kuchangia upatikanaji wa chakula, fedha za kigeni na pato la taifa. Aidha, sekta ndogo ya nyama imewezesha nchi kutotumia akiba ya fedha zake za kigeni kuagiza nyama toka nje. Michango hii inatokana na juhudi za wafugaji wenyewe wadau na serikali kukazana katika kuendeleza sekta hii ndogo ya nyama.

Ndugu Mwenyekiti, tutakubaliana kwamba bado kuna fursa kubwa ya kuongeza uzalishaji endapo mbinu za kuendeleza malisho, kufuga mifugo bora zaidi, kudhibiti magonjwa pamoja kulenga uzalishaji unaozingatia mahitaji ya soko. Serikali itaendelea kuhamasisha wadau kuwekeza katika ufugaji wenye tija na wa kibiashara ili kuinua kipato cha wafugaji, hivyo kuchangia katika Mkakati wa Taifa wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUKUTA).

Pia, napenda kuwapongeza wafugaji wote hususan wafugaji wa asili kwa kuiendeleza sekta ndogo hii licha ya changamoto nilizozitaja hapo juu. Juhudi za wafugaji wa asili zinachangia soko la nyama kwa zaidi ya asili mia 90.

Ndugu mwenyekiti, kuna usemi usemao kuwa *nyama yote ni majani* kwa maana ya kwamba ubora wa nyama hutegemea sana ubora wa malisho. Wingi na ubora wa malisho ndio msingi wa ubora wa nyama, na hivyo Baraza lako halina budi kushauri wadau wa nyama kusaidia kutoa elimu kwa wafugaji juu kuendeleza malisho. Malisho yaliyoko ni ya asili na wingi na ubora wake hupungua kulingana na msimu wakati mbinu za uzalishaji, uvunaji na hifadhi hazijaboreshwa na uwekezaji katika eneo hili ni mdogo.

Napenda kutoa wito kwa Halmashauri za wilaya hususan zile zilizoko katika kanda zenye mifugo, kuhimiza maendeleo ya malisho kwa lengo la kuboresha lishe ya mifugo na hatimaye kuongeza ubora wa nyama. Wizara yangu itaendelea kuhakikisha mbegu bora za malisho pamoja na mbegu bora ya mifugo wa nyama zinapatikana ile kuendeleza sekta ya mifugo kwa ujumla na kipekee kuendeleza sekta ndogo ya nyama.

Ndugu Mwenyekiti, ninafahamu kwamba vipo viwanda/machinjio takribani saba vidogo na vya kati vya kuchinja na kusindika nyama na bidhaa zake. Viwanda hivyo ni pamoja na *Arusha Meat Company* (ng'ombe 150 na mbuzi 200), *Tanzania Meat Company* - Dodoma (ng'ombe **200** na mbuzi **200**), SAAFI - Sumbawanga (ng'ombe **225** na mbuzi **400**), *Tanzania Pride Meat* (ng'ombe **150** na kondoo **200**, kuku **8,000**), Interchick (kuku **3,000**), Mkuza; TANMEAT 2002 Ltd, Dar es Salaam (kinasindika **tani 1** kwa siku), Happy Sausage - Arusha (ng'ombe **80** kwa wiki). Juhudi za Serikali na sekta binafsi kuwekeza kwenye machinjio/viwanda vya kusindika nyama zinaendelea ambapo unahusisha ujenzi wa machinjio ya Ruvu ambayo itakapokamilika itakuwa na uwezo wa kuchinja ng'ombe **800** na mbuzi **400** kwa siku na machinjio ya Manyara Ranchi itakayokuwa na uwezo wa kuchinja ng'ombe **100** na mbuzi **200** kwa siku.

Ndugu Mwenyekiti, ninafahamu kwamba pamoja na ongezeko la viwanda vya kusindika na kuongeza thamani zao la nyama, uwekezaji mdogo unaotokana na uwezo mdogo kimitaji, teknolojia duni, mfumo hafifu wa upashanaji habari na ushirikiano kati ya wadau mbalimbali imekuwa changamoto kubwa kwa maendeleo ya viwanda vya kusindika na kufungasha nyama. Kushindwa kuendeleza ranchi ndogo ndogo zilizogawiwa kwa wawekezaji wa ndani na usindikaji wa chini ya uwezo wa kiwanda katika

viwanda vilivyopo ambapo mifano ni SAAFI **(50%)**, Arusha Meat Company **(50%)**, TANMEAT 2002 **(10%)**, Interchick (50%), Tanzania Meat Company **(50%)**. Aidha, uzalishaji wa nyama kwa kiwango cha chini cha ubora katika machinjio za Halmashauri na kufungwa kwa viwanda vya Tanzania Pride Meat cha Morogoro ni baadhi tu ya changamoto zilizopo. Jambo hili linakwamisha maendeleo ya usindikaji na uongezaji wa thamani wa zao la nyama, Ni vema tukajiuliza kuwa hali hii itaendelea mpaka lini? Wakati sasa umefika kwa kila mmoja wetu kujiangalia katika nafasi yake na kuona namna atakavyoweza anaweza kuchangia katika kuongeza mchango wa sekta katika pato la Taifa. Ninaamini kwamba mkutano huu wa tatu wa ngazi ya juu ya maamuzi utaliangalia suala hili kwa undani na kuweka mkakati wa kuinusuru sekta hii muhimu.

Ndugu Mwenyekiti, Baraza lako pamoja na Bodi ni vyombo vilivyoundwa kisheria ili viwe jukwaa la wadau katika kutetea maslahi muhimu ya wadau na masuala yanayojitokeza katika uendelezaji wa sekta na kushawishi mabadiliko katika nyanja mbali mbali za kiutendaji. Sheria ya Nyama Na 10 ya Mwaka 2006 inahimiza kuwepo wa vyama vya wadau vyenye nguvu katika ngazi ya Taifa kama sehemu ya juhudi za serikali kujenga mazingira ya kuwezesha wadau kushirikiana na serikali katika kuleta maendeleo ya sekta kwa kuwezesha kuwepo kwa *Public Private Dialog*. Kutokana na umuhimu wa vyama vya wadau serikali imaainisha suala hili katika Ilani ya uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi kama nilivyoanisha hapo juu. Nimeelezwa kwamba katika baraza hili wapo wawakilishi wa vyama ambavyo sio hai. Napenda kuwakumbusha wadau wa sekta hii kwamba vyama vilivyo imara ni vile vyenye uwezo wa kifedha, vinavyofanya mikutano yake kwa mujibu wa katiba, vinavyohamasisha ushiriki wa wanachama wake katika shughuli mbali mbali za maendeleo na vinavyoweza kushawishi na kutetea hoja za maendeleo ya sekta katika majukwaa mbali mbali.

Hivyo basi, naagiza kwamba vyama hivyo vifufuliwe na kuimarishwa kwa kujengewa uwezo ili viweze kutekeleza majukumu yake. Ni kwa kushirikiana tu ndipo tutaweza kuweka na kuimarisha mfumo wa uzalishaji na kuongezea thamani zao la nyama kwa kuweka mawasiliano ya kibiashara kati ya wafugaji, wafanyabiashara, wasindikaji na walaji mawasiliano yatakayowezesha wadau kupeana mrejesho chanya katika jitihada za kuzalisha mifugo bora, nyama na bidhaa za nyama zenye ubora unaokidhi mahitaji ya soko na kumfikia mlaji kwa wakati. Kufanya hivyo tutawezesha kuwa na biashara inayohimili ushindani na

kutoa ushawishi kwa watanzania walio wengi kula nyama bora, safi na salama kwa lengo la kujenga afya zao na kukuza soko la ndani la nyama.

Katika kuendeleza na kukuza nyama nchini, sera ya Taifa ya Mifugo ya mwaka 2006, inatoa maelekezo kwamba: (1) uendelezaji wa koo bora za ng'ombe kwa ajili ya nyama; (2) uboreshaji wa koosaafu kwenye ng'ombe wa asili; (3) Serikali kuwezesha na kuimarisha utoaji wa huduma za kitaalam; (4) kuhamasisha juu ya uanzishwaji wa vyama vya kifugaji; (5) kuanzisha mfumo wa utambuzi, usajili na ufuatiliaji wa mifugo na mazao yake.

Ndugu Mwenyekiti, ninapenda pia nikumbushe baraza lako juu ya Ilani ya uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010 - 2015 inayotuagiza kuongeza mchango wa sekta ya mifugo katika pato la Taifa na nina nukuu:

i. *"Serikali isimamie kwa ufanisi mkubwa mradi wa kopa ng'ombe, lipa ng'ombe kama hatua ya kueneza ufugaji wa kisasa wenye tija kubwa;*
ii. *Kuendeleza elimu kwa wafugaji ili wajue kuwa mifugo waliyonayo ni mali inayoweza kuvunwa katika umri na uzito muafaka unaokidhi mahitaji ya soko, ili kuwaondolea umaskini wao badala ya kuridhika na wingi wa mifugo iliyo duni na maisha ya kuhamahama;*
iii. *Uzalishaji wa mitamba upanuliwe kwa kiwango kikubwa kwa Serikali kuivutia na kuwezesha sekta binafsi katika uzalishaji na ufugaji wa kisasa;*
iv. *Kuongeza na kuimarisha vituo vya uzalishaji mbegu bora za mifugo na kuhimiza matumizi ya mbegu hizo;*
v. *Kuhamasisha uanzishaji na uimarishaji wa vikundi vya ushirika wa wafugaji"* mwisho wa kunukuu.

Ndugu Mwenyekiti, katika juhudi za Serikali kuhakisha kuwa sekta za kilimo na mifugo zinachangia kikamilifu kupunguza au kuondoa kabisa umaskini kwa Watanzania imetunga sera na mikakati ya kuleta mapinduzi ya kilimo hapa nchini na utekelezaji wake unasisitizwa na azma ya 'KILIMO KWANZA' kupitia nguzo zake kumi zilivyoanishwa katika azma hiyo, naomba kuzinukuu kama ifuatavyo;

i. *"Utashi wa kisiasa kutoa msukumo wa mapinduzi ya Kilimo;*
ii. *Kugharamia mapinduzi ya Kilimo;*
iii. *Uboreshaji wa mfumo wa utawala wa kilimo;*
iv. *Mabadiliko ya mfumo mkakati katika kilimo;*

v. *Upatikanaji wa ardhi kwa ajili ya kilimo;*
vi. *Vivutio vya kuchochea uwekezaji katika kilimo;*
vii. *Uendelezaji wa viwanda katika kuleta mapinduzi ya kilimo;*
viii. *Sayansi, Teknolojia na Rasilimali Watu katika kuwezesha mapinduzi ya kilimo;*
ix. *Uendelezaji wa Miundombinu ili kuwezesha mapinduzi ya kilimo;*
x. *Uhamasishaji na ushirikishwaji wa Watanzania kuunga mkono na kutekeleza "**KILIMO KWANZA".***

Ndugu Mwenyekiti, njia pekee ya kuchangia juhudi za Serikali za kupunguza umaskini ni kuhamasisha wafugaji kuvuna mifugo yao na kuwaelimisha wadau juu ya uzalishaji wa zao la nyama unaozingatia kanuni za uzalishaji bora. Aidha, ufugaji wa kibiashara unaoendeshwa katika Ranchi za Taifa na za wawekezaji binafsi wakiwemo, wawekezaji waliomilikishwa vitalu kutoka Ranchi za Taifa unawakilisha takribani **asilimia 2** tu ya mifugo yote hapa nchini. Hata hivyo, uzalishaji wa mifugo bora na nyama unakabiliwa na changamoto nyingi ikiwa ni pamoja na;-

i. upatikanaji wa mbegu bora za mifugo ya nyama,
ii. uvunaji wa mifugo kwa wakati,
iii. uzalishaji wa nyama inayokidhi viwango vya ubora kulingana na mahitaji ya soko,
iv. upatikanaji na matumizi bora ya ardhi,
v. mifumo bora ya uzalishaji wa mifugo ya nyama,
vi. upatikanaji na uhifadhi wa malisho bora na maji ya kutosha,
vii. udhibiti wa magonjwa,
viii. upatikanaji wa mtaji,
ix. upatikanaji na matumizi ya miundombinu muhimu kwa ufugaji,
x. utaalamu wa ufugaji, na
xi. uwezo wa kukidhi mahitaji ya soko la ndani na la nje.

Ndugu Mwenyekiti, nafahamu kwamba majukumu ya Baraza hili yanaratibiwa na Bodi ya Nyama Tanzania, Bodi inayoundwa na wadau wenyewe, hivyo ni budi kuzingatia uzoefu wenu na mazingira ya sasa ya utandawazi katika uchumi wa soko na ushindani wa kibiashara katika kuiwezesha Bodi kutoa uwakilishi madhubuti wenye mtazamo wa kibiashara utakaotuwezesha kupata masoko ya kuaminika na endelevu.

Ndugu Mwenyekiti, mwisho, napenda kuyawekea mkazo mambo yafuatayo:

- Uzalishaji na uongezaji thamani wa zao la nyama uzingatie viwango vya ubora kwa mujibu wa sheria na kanuni zake. Hatua kali zichukuliwe dhidi ya wadau watakaokiuka taratibu husika;
- Nyama na bidhaa zake zinazoingizwa kutoka nje ya nchi zidhibitiwe ili kuwa na ushindani wa haki wa kibiashara utakaochochea maendeleo endelevu ya sekta ndogo ya nyama;
- Vyama vya wadau viundwe, vifufuliwe na kuimarishwa kwa kujengewa uwezo;
- Kuhamasisha uundaji wa SACCOS ili kutoa fursa ya kupata mitaji.
- Kuhamasisha wadau kuingia ubia na wawekezaji wengine;
- Kuboresha mifugo kwa kutumia uhimilishaji ili kupata mifugo bora.

Ndugu Mwenyekiti, narudia tena kusema kuwa, maendeleo ya sekta ya nyama yanategemea hamasa ya wadau kuingia kwenye ufugaji wa kibiashara, iwe ni watu binafsi, makampuni au vikundi. Aidha, napenda niwakumbushe kwamba ufugaji unaoweza kutuletea tija ni ule wa Ranchi wenye uwezo wa kuzalisha mifugo bora iliyo huru na magonjwa.

Ndugu Mwenyekiti, ni matarajio yangu kwamba Baraza hili litatathmini utekelezaji wa yale yaliyoelekezwa katika Mkutano wa **Pili wa Baraza** na kuainisha changamoto ili zijadiliwe na kupatiwa ufumbuzi. Vile vile litatoa maazimio yatakayowezesha kupunguza au kuondoa kabisa vikwazo katika kuendeleza sekta ya nyama na hivyo kuongeza mchango wake katika pato la Taifa. Hivyo, nawatakia mkutano mwema wenye ufanisi na mafanikio makubwa. Baada ya kusema hayo, napenda sasa kutamka kuwa mkutano wa tatu wa Baraza la Mwaka la Wadau wa Sekta ya Nyama **umefunguliwa rasmi**.

ASANTENI KWA KUNISIKILIZA